




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO



Kumb,Na. KTV/NDC/P. 30/2/44

17.07.2023.

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI (MARUDIO).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo anapenda kuwatangazia nafasi za Kazi Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi ya **Mwendesha Ofisi Daraja la II**, nafasi tano (5) za ajira ya Masharti ya kudumu. Tangazo hili ni baada ya kupokea kibali cha ajira chenye Kumb.Na.FA.97/228/01" TEMP"/06 cha tarehe **06 April, 2023** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kibali hiki ni kutekeleza lkama na bajetii kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

1. MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA LA II – NAFASI 5

MAJUKUMU YA KAZI

- i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasilisha shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake Majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo Ofisini
- v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake, pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe ametihimu Elimu ya Kidato cha Nne au Sita (IV, VI) mwenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au Cheti cha NTA level Six (6) ya Uhazili. Aidha, awe wamefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kingereza maneno mia moja (100) kwa dakika moja na kupata program za Komputa za Ofisi kama vile:- Word, Excel, Powerpoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali

MSHAHARA


Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Serikali yaani **TGS C** kwa mwezi.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Muombaji awe raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya wilaya Nsimbo.
- ii. Muombaji awe na umri kati ya miaka 18 na usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- iii. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Details CV) namba za simu na Anwani sahihi na wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.
- iv. Maombi yote ya muombaji yaambatane na nakala za Vyeti vya taaluma, Vyeti vya Kidato cha Nne au sita (IV au VI), Cheti cha kuzaliwa, cheti cha NIDA au namba na picha moja (1) za passport size za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- v. Testimonials na "Provisional statement of results" hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na sita **HAVITAKUBALIWA**.
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na mamlaka husika (TCU na NACTE) na taarifa ya ulinganishi iambatanishwe kwenye maombi.
- vii. Siku ya usaili kila muombaji afike na vyeti halisi (Original Certificates).
- viii. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi waombaji wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
- ix. Maombi yasiyozingatia sifa zilizo rodheshwa hayata shughulikiwa
- x. Waombaji waliostafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawataruhusiwa kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- xi. Waombaji wote watakaokithi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili.
- xii. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 30/07/2023 saa 9.30 Alasiri
- xiii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta kwa Anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Nsimbo,
S. L. P 688,
MPANDA.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo yenye www.nsimbodc.go.tz


Erinckwas .T. John
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA NSIMBO**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO**

Nakala: Katibu,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
S. L. P 2320,
DODOMA.